HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE | TOLEO LA 006 | JULAI 2023 | HALIUZWI

Jarida la

# TEMEKE YETU

FAHAMU ZAIDI



## KARIBU TEMEKE MHE. MOBHARE MATINYI - MKUU MPYA WA WILAYA YA TEMEKE.

HABARI KAMILI UK. 1




## RAIS SAMIA AONGOZA MAPOKEZI YA BOEING

Ameungana na viongozi mbalimbali wa Nchi, Chama na Wananchi kupokea na kukagua ndege ya mizigo aina Boeing 767-300F katika uwanja wa ndege wa Kimataifa Julius Kambarage Nyerere.

HABARI KAMILI UK. 3

MHARIRI MKUU

**FRANCISCA MSELEMU**

Kaimu Mkuu - Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Manispaa ya Temeke

WAHARIRI WASAIDIZI

**SWEETBETTER NJIGE**

Afisa Habari - Manispaa ya Temeke

**SHALUA MPANDA**

Afisa Habari - Manispaa ya Temeke

WAPIGA PICHA

**METHEW JONAS**

Afisa Habari - Manispaa ya Temeke

**GERVAS EDICK**

Afisa Habari - Manispaa ya Temeke

MSANIFU WA JARIDA

**MICHOLAX MUSSA**

Afisa TEHAMA - Manispaa ya Temeke



# KARIBU TEMEKE MHESHIMIWA MOBHARE MATINYI - MKUU MPYA WA WILAYA YA TEMEKE.

Na Sweetbetter Njige

Aliyekuwa mkuu wa wilaya ya Temeke, Bi.Mwanahamisi Munkunda leo Julai 4, 2023 amekabidhi ofisi kwa mkuu mpya wa wilaya mheshimiwa Mobhare Holmes Matinyi.

Wakati wa makabidhiano hayo, Bi Mwanahamisi Munkunda ameshukuru uongozi wa manispaa ya Temeke kwa ushirikiano na amemuhakikishia ushirikiano Mkuu huyo mpya wa wilaya.

"Nashukuru nimetengeneza marafiki wengi Temeke na jambo jema naiacha Temeke ikiwa salama". Alisema Bi.Munkunda

Kwa upande wake mkuu wa wilaya ya Temeke Mhe.Mobhare Matinyi amemshukuru Bi Munkunda na kuahidi kuendeleza yale yote mazuri aliyoyakuta huku akiwataka watendaji wa manispaa hii kumpa ushirikiano.

Hafla hiyo fupi ya makabidhiano pia ilihudhuriwa na Mstahiki meya wa manispaa hii Mhe.Abdallah Mtinika,Mkurugenzi wa Manispaa ndugu Elihuruma Mabelya, Mbunge wa Jimbo la Temeke Mhe.Dorothy Kilave pamoja na wajumbe wengine wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.





# RC CHALAMILA ASHIRIKI BARAZA LA MADIWANI.

Na Sweetbetter Njige

Kikao cha Baraza la madiwani pamoja na Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mhe.Albert Chalamila kilifanyika katika Ukumbi wa Iddi Nyundo Juni 23,2023.

Kikao hiki cha kupitia hoja muhimu zilizoibuliwa na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG) pia kimehudhuriwa na Mkuu wa wilaya ya Temeke Mhe. Mwanahamisi Munkunda, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke Mhe. Abdallah Mtinika, Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Ndg. Elihuruma Mabelya,



Mbunge wa Jimbo la Temeke Mhe. Dorothy Kilave pamoja na wajumbe wengine wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

***"Temeke tutaendelea kusimamia misngi ya utawala bora na matumizi mazuri ya mapato yetu ya ndani"*** -
*Mhe. Abdallah Mtinika, Meya wa Manispaa.*



# NAIBU WAZIRI NDEJEMBI:TUTAFANYIA KAZI CHANGAMOTO YA UKOSEFU WA MAENEO YA UJENZI WA SHULE TEMEKE.

Na Shalua Mpanda

Deogratias Ndejembi amefanya ziara kukagua miradi mbalimbali ya elimu inayotekelezwa wilayani Temeke.

Katika ziara hiyo ya kukagua miradi ya elimu kwa upande wa shule za Msingi na Sekondari, Mhe.Ndejembi amesema halmashauri ya Temeke imekuwa ikipokea fedha nyingi za
miradi ya elimu kutoka Serikali kuu ambapo kwa mwaka uliopita ilipokea zaidi ya milioni 400 ila changamoto kubwa ni ufinyu wa maeneo ya ujenzi wa madarasa.
"Tunatambua kuwa kuna changamoto ya maeneo na hili ni tatizo la mkoa mzima wa Dar es
salaam ndio maana tunapendekeza ujenzi wa shule za ghorofa na sisi kama Ofisi ya Rais
tutakwenda kukaa tuje na michoro maalum kwa ajili ya mkoa wa Dar es salaam na manispaa zake". Alisema Naibu Waziri huyo

Aidha Mhe.Ndejembi amewataka viongozi wa manispaa ya Temeke kukamilisha ujenzi wa shule ya Sekondari Dovya kwa muda waliokubaliana Ili kuwezesha wanafunzi wa kidato cha kwanza waweze kuyatumia.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri huyo aliongizana na Mkuu wa wilaya ya Temeke Mhe.Mobhare Matinyi,Meya wa manispaa ya Temeke Mhe.Abdallah Mtinika,waheshimiwa wabunge wa majimbo ya Mbagala(Abdallah Chaurembo) na Temeke(Dorothy Kilave), Mkurugenzi wa Manispaa hii ndugu Elihuruma Mabelya na viongozi wengine wakiwemo wa Chama Tawala(CCM).




# WALINDENI WATOTO WENU DHIDI YA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA - MHE. ABDALLAH MTINIKA.

Na Shalua Mpanda

Wito umetolewa kwa wazazi kuhakikisha maendeleo ya Teknolojia hayachangii katika mmomonyoko wa maadili katika Jamii hususan kwa watoto.

Wito huo umetolewa na Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke mheshimiwa Abdallah Mtinika wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambapo kiwilaya yamefanyika Juni 16,2023 katika shule ya Sekondari Kibasila.

Mhe.Mtinika amesema kuwa wazazi wengi wamekuwa na tabia za kuwaruhusu watoto wao kutumia vifaa vya kielektroniki kama vile simu, kompyuta pamoja na runinga bila kufuatilia maudhui wanayoyatazama kwenye vifaa hivyo. "Vifaa hivi vikitumiwa vizuri ni msaada mkubwa sana katika kumuendeleza mtoto kielimu lakini wengi wetu tumekuwa na tabia za kuwapa uhuru vijana wetu kuvitumia bila kuwa na uangalizi". Alisema Mtinika

Pia amesisitiza wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni na kujenga tabia ya kuongea nao mara kwa mara ili kuweza kutambua changamoto zao.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Temeke Mhe.Dorothy Kilave amewataka wazazi kuwafichua wale wote wanaowafanyia vitendo vya kikatili watoto na kuacha tabia za kufichiana siri ili kuweza kuwanusuru watoto dhidi ya vitendo hivyo.

Maadhimisho hayo ya Siku ya Mtoto wa Afrika hufanyika kila Juni 16 kila mwaka kukumbuka vifovya mamia ya watoto waliouwawa na makaburu huko nchini Afrika ya Kusini katika mji wa Soweto Juni 1976 wakati walipoandamana kudai haki zao ikiwemo ya elimu.






# RAIS SAMIA AONGOZA MAPOKEZI YA BOEING 767-300F.

Na Sweetbetter Njige

Ameungangana na viongozi mbalimbali wa Nchi, Chama na Wananchi kupokea na kukagua ndege ya mizigo aina Boeing 767-300F katika uwanja wa ndege wa Kimataifa Julius Kambarage Nyerere.

Ndege hiyo yenye uwezo wa kubeba zaidi ya tani 50 za mizigo itapunguza changamoto za usafirishaji zilizokua zinawakabili wafanyabiashara Nchini kwa kuwawezesha kusafirisha mizigo yao ndani na nje ya Nchi kwa gharama nafuu na kwa wakati.




***Mpaka sasa ATCL (kampuni ya ndege Tanzania) imefikisha jumla ya ndege 13 nyingine tatu zikiwa matengenezoni.***

Serikali ya Tanzania inaendelea kufanya uwekezaji katika sekta ya usafirishaji wa anga ili kuendana na ushindani wa kibiashara katika soko la kimataifa.



# "ASANTENI SANA WALIMU" - DC MUNKUNDA.

Na Sweetbetter Njige

Shule za msingi na Sekondari wa Wilaya hii kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Ameyasema hayo leo Juni 6,2023 katika viwanja vya Ofisi ya manispaa Temeke wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo kwa shule,walimu na wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao.

Mhe.Munkunda amesema kazi inayofanywa na walimu ni kubwa na ngumu lakini wamekuwa wakifanya kazi hiyo kwa moyo na kujituma na kama uongozi unatambua mchango wao.

"Niwapongeze sana walimu na sina neno kubwa la kusema zaidi ya ahsante, Ahsanteni sana walimu na Mkurugenzi na Mstahiki meya muone namna ya kuweza kuwapa motisha zaidi walimu hawa kwa kazi wanayoifanya.

Naye Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke Abdallah Mtinika amesema Baraza la madiwani lipo tayari kufikiria namna ya kuwaongezea motisha walimu wanaofanya vizuri ili kuwatia moyowalimu hao.

Akitoa taarifa ya elimu katika Wilaya hii kwa mkuu wa wa Wilaya,Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amesema wataendelea kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kujenga vyumba zaidi vya madarasa na matundu ya vyoo.

Manispaa ya Temeke imejiwekea utaratibu wa kutoa tuzo hizo kila mwaka kwa ajili ya kuwapa motisha walimu na wanafunzi ili kuendelea kuinua kiwango cha ufaulu katika Manispaa hii.



# OFISI ZA SERIKALI SIO VITUO VYA KUKUSANYIA MAPATO - DC MUNKUNDA.

Na Shalua Mpanda

Madaraka yao kinyume na taratibu za utumishi wa Umma kuacha tabia hizo na kuwahudumia wananchi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

Wito huo umetolewa na mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda Juni 15,2023 wakati wa ziara ya kuzungumza na wananchi katika kata ya Azimio.

Mhe.Munkunda amewataka watendaji wa Serikali za Mitaa na watumishi wengine kutatua kero na changamoto kwa wananchi na kutambua nafasi walizokuwa nazo wamezipata kwa lengo la kuwasaidia wananchi na sio kwa maslahi yao binafsi. "Sikilizeni kero zao na kuzitatua,mnapata mishahara kwa kazi hiyo, haukufuatwa nyumbani kuombwa kufanya kazi hii.....na huduma katika Ofisi hizi ni bure msigeuze ofisi zenu kama vituo vya kukusanyia mapato". Alisisitiza Mkuu huyo wa Wilaya.

Katika mkutano huo moja ya hoja iliyoibuliwa na wakazi wa kata hiyo ya Azimio ni suala la baadhi ya askari kutokuwa waaminifu na kutokufuata taratibu za kazi ambapo mkuu wa Jeshi la Polisi wilaya ya Chang'ombe Mrakibu wa Polisi Godfrey Mkangale ameahidi kulitafutia ufumbuzi wa haraka.

Ziara ya kata kwa kata yenye lengo la kutembelea kata zote 23 ndani ya wilaya ya Temeke iliyoanzishwa na Mkuu huyo wa Wilaya ina lengo la kusikiliza changamoto mbalimbali na kujitambulisha kwa wananchi.



# DC MUNKUNDA ATOA MAELEKEZO KWA MKANDARASI UJENZI HOSPITALI RANGI TATU.

Na Shalua Mpanda

Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda amemtaka mkandarasi kampuni ya Group Six International iliyopewa kandarasi ya upanuzi wa hospitali ya Mbagala Rangitatu kukamilisha kazi hiyo kwa wakati.Ametoa agizo hilo leo Juni 5,2023 wakati wa hafla ya utiaji saini wa makubaliano ya ujenzi huo wa jengo la ghorofa 6 ambapo mpaka kukamilika kwake unatarajia kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 10.4.

Mkuu huyo wa Wilaya amesema Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 2 za kuanza kwa ujenzi huo hivyo hatarajii kuona kazi hiyo ikichelewa kuanza. "Mradi huu kwetu ni ahsante kwa Mhe.Rais, tunaomba umpe heshima yake ikiwezekana mradi huu ukamilike kabla ya miezi hiyo 24".Alisisitiza Mhe.Munkunda




Awali akimkaribisha mkuu wa Wilaya, Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke Mhe. Abdallah Mtinika ametoa wito kwa Wananchi kuendelea kulipa kodi na tozo mbalimbali zitakazoiwezesha Halmashauri kupata fedha za kukamilisha miradi mbalimbali.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amemuhakikishia mkuu wa Wilaya kuwa ataendelea kusimamia fedha za Serikali kikamilifu ili ujenzi huo uendane na thamani halisi ya fedha.

Ujenzi huo wa jengo hilo la ghorofa 6 utakapokamilika utasaidia kuondoa msongamano wa wagonjwa hospitalini hapo na kusaidia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za afya kwa wakazi wa wilaya ya Temeke na hata wilaya za jirani.



# MFUKO WA FARAJA TEMEKE WAKABIDHI HUNDI KWA WANACHAMA 13.

Na Sweetbetter Njige

Kaimu mkurugenzi wa maispaa ya Temeke wakili Faraja Nakua amekabidhi hundi kwa Wanachama 13 wa mfuko wa faraja waliofikwa na matatizo mbalimbali kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa mfuko huo.


Akikabidhi hundi hizo Wakili Nakua amempongeza mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya na afisa utumishi na idara yake kwa kuasisi mfuko huo na kueleza kuwa mfuko huu utaenda kuwa faraja kubwa kwa Wanachama.

"Hivi leo tunaona matokeo haya ni kwa kuwa kuna watu waliwaza, nimpongeze afisa utumishi na
idara yake kwa kufanya kwa vitendo, najua hiki kinachotolewa hapa hakiwezi kwenda kufidia
umuhimu wa mliowapoteza lakini ni faraja kukumbukwa na Wanachama wenzako japo kwa hiki kidogo, nikupongeze mwenyekiti wa mfuko, tumeanza kuona matunda, watu wataona amana yao ipo salama na inaleta matokeo, muendelee kuwa na uaminifu huo huo"

Kwa upande wake afisa utumishi manispaa ya Temeke ndugu Bihaga Yogwa ametoa pole kwa waliofikwa na changamoto na kupongeza viongozi wa mfuko kwa kuanza zoezi hilo. Alisema "Leo rasmi mfuko unaonekana kwa vitendo, nishukuru Menejimenti kwa kuridhia tuwe na mfuko huu, mfuko huu unaenda kusaidia mtumishi anapata tatizo kwa wale ndugu/wategemezi ambao hawaguswi na sheria za utumishi wa umma, na kutoa mikopo midogo midogo na kupunguza adha kwa watumishi wenzetu, unapopata shida ukaguswa na wa karibu yako inakua faraja sana na hilo ni muhimu sana" Akieleza malengo ya mfuko huo mwenyekiti wa mfuko ndugu Suleman Ame alisema mfuko unalenga kuwasaidia Wanachama kupata mikopo midogo midogo yanye riba nafuu, kusaidiana katika matatizo ambapo Mfuko unaweza kumsaidia Mwanachama hai kupata hadi kiasi cha shilingi Milioni moja (1,000,000/=) ndani ya masaa 24 baada ya kupata tatizo.

Mfuko wa Faraja ulianzishwa mwezi Oktoba 2022 ambapo kufikia mwezi Novemba 2022 Wanachama hai walianza kushiriki kuchangia mfuko huo na mpaka sasa mfuko una jumla ya Wanamchama 1,668 ambapo kati yao Wanachama 12 wamefiwa na 1 kufariki.

**JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA**
OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**




# HATUA ZA KUKATA LESENI KWA MFUMO MPYA WA TAUSI

**Mfumo huu unapatikana kwenye anwani ya tovuti:**
**tausi.tamisemi.go.tz**

## 1. USAJLI (REGISTRATION)

- Namba ya NIDA (NIN)
- Namba ya simu iliyosajiliwa kwa namba ya NIDA
- E - Mail Address

## 2. MAOMBI YA LESENI (APPLICATION FOR LICENCE)

### A. MAOMBI BINAFSI

- TIN namba
- Mkataba wapango/ hati ya eneo
- Tax clearance

### B. KAMPUNI

- TIN namba
- Mkataba wa pango/ Hati ya eneo
- Tax clearance
- TIN namba ya mwakilishi wa kampuni (care taker)
- Memorundum
- Certificate of incorporatio
- Namba ya NIDA ya mwakilishiwa kampuni (care taker)

KWA MAELEZO ZAIDI TUPIGIE SASA;
**0715 415 250 | 0783 399 423 | 0714 306 833**



# TARURA TEMEKE YATAMBULISHA MRADI DMDP AWAMU YA 2.

Na Sweetbetter Njige

Meneja wa TARURA wilaya ya Temeke mhandisi Paul Mhere ametambulisha rasmi Mradi wa Ue delezaji na Uboreshaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP) awamu ya pili utakaowezeshwa na fedha kutoka benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika maeneo muhimu kwa uchumi wa jamii.

Akieleza ujio wa mradi huo Mhandisi Mhere alisema ushirikishwaji wa Viongozi na Jamii ni hatua ya kwanza muhimu kuelekea utekelezaji huo.

"Leo tumekua na waheshimiwa madiwani, wakuu wa idara,vitengo, wageni kutoka TAMISEMI, wadau mbalimbali lengo kubwa ni kutambulisha mradi wa Uendelezaji na Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam awamu ya pili, mradi utakaokwenda kugusa maeneo mbalimbali,utakua na 'components' kuu 4, miundombinu (Barabara, Zahanati,Shule,-Masoko) kutakua na masuala ya taka ngumu, kujenga uwezo kwa watendaji hasa wanaohudumia mradi, na Usimamizi wa mradi. Tunashukuru Madiwani wameupokea mradi vizuri na shukrani nyingi zimekwenda kwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan"

Mradi wa DMDP awamu ya pili unatarajiwa kugharimu dola za kimarekani milioni 350,000,000.00/= (kwa miradi yote itakayotelezwa Dar es Salaam) kwa maeneo yote manne (Miundombinu dola za kimarekani milioni 256,000,000/=, Taka ngumu dola milioni 50,000,000/=, Kujenga Uwezo kwa watendaji dola milioni 28.3 na Usimamizi wa miradi dola za kimarekani dola za Kimarekani milioni 15.7).

Mgawanyo huo unaipa manispaa ya Temeke kupitia jimbo la Temeke jumla ya kilometa za barabara zilizopendekezwa 64.07, jimbo la Mbagala kilometa 112.46, Temeke imependekeza soko 1 (soko la Keko) mifereji ya maji yenye urefu wa kilomita 11.6 na kilomita 8.4 kwa jimbo la Mbagala), makaravati na vivuko ( Temeke vivuko 6 na Jimbo la Mbagala makaravati makubwa 4).

Kwa makisio wilaya ya Temeke kwa ujumla inatarajia kupata dola za Kimarekani milioni 146.65.



# DC TEMEKE AWATAKA VIJANA KUTUMIA CHANGAMOTO ZILIZOPO KUWA FURSA.

Na Shalua Mpanda

Kubadili changamoto iliyopo ya ukosefu wa ajira na kuwa fursa. Ameyasema hayo alipotembelea kituo cha kutolea huduma za afya(Polyclinic) cha JPG kilichopo kata ya Chang'ombe wilayani Temeke.

Akiwa katika kituo hicho kinachomilikiwa na vijana waliowezeshwa mkopo wa aslimia 10 na manispaa ya Temeke,Mhe.Mtinyi amewataka vijana kutokusubiri ajira za Serikali na badala yake wajiajiri kama walivyofanya vijana hao.

"Nimekuja kuwapongeza kwa juhudi mlizofanya,Sekta yetu ya elimu inazalisha wataalamu mbalimbali wenye ujuzi lakini bado soko la ajira halijaweza kuwachukua wote,tunapopata vijana wenye juhudi kama zenu tunapata faraja kubwa".Alisema Mkuu huyo wa Wilaya

Awali muwakilishi wa Vijna hao akisoma taarifa kwa Mkuu wa wilaya,alisema waliona changamoto ya upatikanaji wa huduma za afya katika eneo hilo wakaunda kikundi na kwenda kuomba mkopo wa aslimia 10 katika ofisi za manispaa ya Temeke na kupewa kiasi cha shilingi milioni 200.

Hii ni ziara ya kwanza ya kikazi ya Mhe.mkuu wa wilaya Mobhare Mtinyi toka ateuliwe na Mhe.Rais Samia Suluhu Hassan kuongoza Wilaya hii akichukua nafasi ya aliyekuwa mkuu wa wilaya Bi. Mwanahamisi Munkunda



# TPA YAKABIDHI VITANDA 15 KWA AJILI YA KINAMAMA TEMEKE HOSPITALI.

Na Sweetbetter Njige

Auni 01,2023 kaimu mkurugenzi wa mamlaka ya bandari Dar es salaam ndugu Mrisho Mrisho amekabidhi jumla ya vitanda 15 vyenye thamani ya shilingi 25,000,000/= kwa mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda ambavyo vitatumika katika wodi za kinamama.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo yaliyofanyika katika viwanja vya hospitali ya Temeke na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali, mhe. Manahamisi Munkunda alisema vitanda hivyo ni faraja kwa wanawake watakaofika kujifungua hospitalini hapo.

"Tumefarijika kupokea vitanda hivi, kwa siku wanawake wanaojifungua hapa kwa rufaa ni 20 mpaka 30, uwepo wa vitanda hivi utawezesha wote kupata huduma kwa wakati mmoja bila kusubiriana na hii inakweda kuthibitisha dhana ya uboreshaji na utoaji huduma mzuri kwa wagonjwa"

Akizungumza kwa niaba ya mkurugenzi mkuu wa mamlaka ya usimamizi wa bandari kaimu mkurugenzi Ndg. Mrisho alisema ni furaha kwa mamlaka hiyo kurudisha kwa jamii hasa katika sekta ya afya kwa kutoa vitanda bora kwa ajili ya kuwezesha zoezi zima la kujifungua kwa kina mama. Kwa upande wake mganga mkuu wa hospitali hiyo daktari Joseph Kimaro alisema

"Tunawashukuru Bandari kwa msaada huu wa vitanda 15 unaokwenda kupunguza changamoto ya vitanda pale wodi ya kujifungua, hii inaakisi ile dhana ya Mhe. Rais ya "Pamoja Tuwavushe Salama" na baada ya kupatikana kwa vitanda tunaamini tutaongeza uhitaji wa huduma"

Mamlaka ya usimamizi wa bandari inaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali na siziso za Kiserikali katika kuhudumia Wananchi wa wilaya ya Temeke kwa kurudisha kwa jamii sehemu ya faidha inayopatikana.




# *Lipa na Tozo kwa maendeleo ya Manispaa yetu.*

# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

***Lilongwe***
***05 Julai, 2023***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Mipango ya Taifa ya Mwaka 2023 pamoja na uamuzi wa kuhamishia masuala ya uwekezaji Ofisi ya Rais, hivyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko madogo ya Miundo ya Wizara na kufanya uteuzi wa viongozi kama ifuatavyo:

1. Ameunda Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambapo amemteua Prof. Kitila Alexander Mkumbo kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Mhe. Prof. Mkumbo ni mbunge wa jimbo la Ubungo.

2. Ameunda Wizara ya Fedha ambapo amemteua Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kuwa Waziri wa Fedha. Kabla ya uteuzi huu Mhe. Dkt. Nchemba alikuwa Waziri wa Fedha na Mipango.

3. Ameunda Wizara ya Viwanda na Biashara ambapo amemteua Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji kuwa Waziri wa wizara hiyo. Kabla ya uteuzi huu Mhe. Dkt. Kijaji alikuwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

4. Amemteua Bw. Lawrence Nyasebwa Mafuru kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ya Taifa. Kabla ya uteuzi huu Bw. Mafuru alikuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango (Usimamizi wa Uchumi).

5. Amemteua Bw. Elijah Mwandumbya kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha (Usimamizi wa Uchumi). Kabla ya uteuzi huu Bw. Mwandumbya alikuwa Kamishna, Idara ya Uchambuzi wa Sera, Wizara ya Fedha na Mipango.




# "USAFI NI MAAGIZO" MHE. MWANAHAMISI.

Na Shalua Mpanda

Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda ameongoza zoezi la usafi wa kila mwisho wa mwezi katika kata ya Kilungule ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya kuweka mkoa wa Dar es salaam katika hali ya usafi.

Akihutubia Wananchi wa kata hiyo ya Kilungule Mhe. Mwanahamisi ameeleza kuwa suala la usafi sio ombi bali ni maagizo na maelekezo ya Serikali na utekelezaji wa ilani chama cha Mapinduzi (CCM). Alisema

"Suala la usafi hatufanyi kwa utashi, ni maelekezo ya Serikali, ni utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi,mwisho wa siku tutaulizwa kwa kuwa tuliwaahidi Wananchi kwamba tutasimamia usafi wa mazingira ili kuepukana na maradhi, lakini kuwapa Wananchi maeneo safi na salama ya kufanya kazi zao. Jambo la usafi liwe ni tabia,tusisubiri Viongozi wapite kwenye mitaa ndio tufanye usafi"

Kwa upande wake mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amemshukuru Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Mhe.daktari Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha kata ya Kilungule kwa utekelezaji wa miradi mikubwa hususani ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali, na kumuahidi diwani wa kata hiyo Mhe. Said Fella kuwa manispaa itaendelea kushirikiana naye ili kumaliza kero zilizosalia.

Naye diwani wa kata hiyo Mhe. Fella amemshukuru mkuu wa wilaya ya Temeke kwa kushiriki usafi wa mwisho wa mwezi na wakazi wa Kilungule na kumuomba kuitembelea kata hiyo katika ziara zake za kata kwa kata ili kuzijua na kuzitatua kero za Wananchi.

Zoezi la usafi wa kila mwisho wa mwezi linalenga kuleta hamasa ya utunzaji wa mazingira kwa Wananchi wa wilaya ya Temeke kuhakikisha mazingira yanasafishwa, kupendezeshwa na kutunzwa kwa usahihi kwa kupanda miti inayofaa ili kupambana na mabadiliko ya tabia nchi na kujikinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko.



# TEMEKE INAENDELEA KUFANIKIWA UTEKELEZAJI MKATABA WA LISHE.

Na Shalua Mpanda

Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mobhare Matinyi ameongoza kikao cha tathmini ya mkataba wa lishe kilichofanyika katika ukumbi wa manispaa( Iddi Nyundo).

Akizungumza katika kikao hicho, Mhe. Matinyi amewataka Watendaji kuwajibika na kuhakikisha kuwa wanatoa taarifa sahihi za utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa kuwa ni Sera ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na ni maagizo ya Mheshimiwa Rais, daktari Samia Suluhu Hassan. Akieleza hali ya lishe mratibu wa lishe manispaa ya Temeke Bi. Happy Nkunda alisema Manispaa imefanya vizuri katika utekelezaji wa mkataba huo,na kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023

utekelezaji wa afua za lishe umeimarika zaidi. Alisema

***“Temeke tumefanya vizuri katika viashiri vingi vya lishe”***

*- Mhe. Mabhore Matinyi, Mkuu wa Wilaya ya Temeke.*

"Tumejadili mambo mbalimbali yaliyopo kwenye mkataba, kwa upande wetu Temeke tumefanya vizuri kwenye viashiria vingi vya lishe. Utekelezaji wa afua za lishe kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umeimarika kutokana na kushirikisha wadau mbalimbali na watendaji kuanzia ngazi ya Kata”

Manispaa ya Temeke inaendelea kusimamia na kutekeleza mkataba wa lishe kwa kuhakikisha Wananchi ikiwemo Wanafunzi wanapata chakula bora hata katika mazingira ya Shule ambako wanasimamiwa kupata chakula kwa ajili ya afya ya mwili na akili.




# WALIMU TEMEKE WAMPONGEZA MKURUGENZI MABELYA.

Na Sweetbetter Njige

Wanachama wa Chama cha Kulinda na kutetea haki za walimu manispaa ya Temeke wamempongeza mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya kwa kuwatua mzigo, kufuatia utekelezaji wa ushauri wa Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Temeke ambapo walishauri kusitishwa makato ya kuchangia vyama viwili vya walimu kinyume na matakwa yao.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Temeke bwana Holle Makungu amesema uamuzi huo umefikiwa kufatia kuwepo na vyama viwili vya walimu ambavyo ni Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na Chama cha Kuwalinda na Kutetea Haki za Walimu (CHAKUHAWATA).

Alisema awali Walimu waliwasilisha malalamiko yao TAKUKURU kuwa wamekuwa wakikatwa mishahara yao na kuchangia Vyama viwili kinyume na kifungu cha 61 (1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya Mwaka 2004 ambayo inampa uhuru mfanyakazi kuchagua makato yake yaelekezwe kwenye Chama gani cha wafanyakazi anachoona kinamfaa.

Ndugu Holle Makungu alibainisha kuwa Kupitia kazi za uzuiaji Rushwa kwa maana ya dhana ya Takukuru rafiki na kwa kuzingatia kifungu cha 7 Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na 11/2007 tulimshauri Mkurugenzi kuhusu kadhia hiyo ambayo imekuwa ikiwapata Walimu hao na baada ya kupata ushauri huo alisitisha mara moja Makato hayo.

PIGA 113



# SAUTI PARASPORT CLUB WAKABIDHI KOMBE MANISPAA YA TEMEKE

Na Sweetbetter Njige

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke Mh.Abdalla Mtinika pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa hii ndg.Elihuruma Mabelya wamepokea kombe la ushindi kutoka kwa timu ya mpira wa miguu ya walemavu -Sauti Parasports Club yenye makazi yake wilayani Temeke.

Akipokea kombe hilo Mh.Abdallah Mtinika amesema Manispaa inawapongeza kwa ushindi huo na kuwaahidi kuwa wataendelea kuwasaidia katika shughulii zao za michezo na wasisite kufika katika ofisi yake pindi watapohitaji msaada wowote, pia amewahimiza kutokukata tamaa kwani wameitangaza vyema Halmashuri na Taifa kwa ujumla.

Timu hiyo ya Sauti parasport Club ilifanikiwa kupata kombe hilo baada ya kuifunga timu ya Mombasa Amputee kutoka Kenya kwa goli 1-0 katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa kwa watu wenye ulemavu.

> ***“Hongera Sana Parasport Club, Temeke tunajivunia ninyi”***
>
> *- Ndg. Elihuruma Mabelya, Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke*

JARIDA HILI HUTOLEWA NA;
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALIN**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**
**S. L.P 46343 TEMEKE, DSM.**
**SIMU: +255 22-2928132**
**NUKUSHI: +255 22-2928137**
**BARUA PEPE: temekemc.go.tz**
**TOVUTI: www.temekemc.go.tz**